**OFISI YA WAZIRI MKUU - TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA KIBAHA**
**SHULE YA SEKONDARI KWALA**

**MKUU WA SHULE 0785-304696**
**MAKAMU MKUU WA SHULE 0788-741109**
**MTAALUMA 0762-459726**
**S.L.P 05**
**MLANDIZI**

**KUMB.NA. KWSS/KDC/1796/J.1/F.5/….** **TAREHE_____________**
MZAZI /MLEZI WA MWANAFUNZI **_____________________________**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO** KATIKA
**SHULE YA SEKONDARI KWALA**

**UTANGULIZI**

Ninayo furaha kubwa ya kukuarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka wa masomo **……….** katikaTahasusi ya **HKL** kwa hiyo anapaswa kuripoti shuleni siku ya tarehe **…………..** kabla ya **saa 11 jioni ya siku za kazi**.

**1. JINSI YA KUFIKA SHULENI**

Shule ipo Kata ya Kwala, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha Mkoa wa Pwani, ili kufika shuleni Ukiwa unatokea **Morogoro** au **Dar es salaam** utashuka kituo cha **Vigwaza sheli**. Alama kubwa ya kuzingatia ni barabara lenye mzunguko (**round about**) na bango kubwa la **SINOTAN** linaloonyesha njia ya kwenda **viwandani/bandari ya nchi kavu ya Kwala**, elekea njia hiyo ya lami hadi kijiji cha Kwala ambapo shule ipo.

**2. MICHANGO YA UENDESHAJI WA SHULE**

Kwa kutekeleza sera ya elimu bila malipo Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania imeondoa Ada, hivyo elimu ni **bila ada** isipokuwa kuna michango midogomidogo ya uendeshaji wa shule kama ilivyoainishwa hapa chini.

| NA | MICHANGO | KIASI |
|---|---|---|
| i | Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| ii | Tahadhari | 5000/= |
| Iii | Nembo | 5000/= |
| iv | Kitambulisho cha Shule | 5000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

**NB**: Hatupokei pesa taslimu, Malipo haya yalipwe kwenye akaunti ya shule iliyoko Bank ya **NMB AKAUNTI NAMBA 21201200102, jina KWALA SEKONDARI**, hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye karatasi ya banki au wakala wa NMB kisha mwanafunzi aje na karatasi ya bank (Bank pay in slip) ili apewe Risiti shuleni wakati wa kuripoti.

**Mawasiliano**

Mawasiliano baina ya MWANAFUNZI na MZAZI/MLEZI yatakuwa kwa **NAMBA RASMI ZA SHULE** na anaweza kutuma fedha kupitia namba hizi na kutoa taarifa fedha aliyoituma ni ya mwanafunzi Fulani

**0654 - 747383 & 0654 – 747398 (KWALA SEC SCHHOL)**

**MUHIMU**

Mahafali ya shule kidato cha sita ni lazima kwa wanafunzi wote wa kidato cha tano na sita kushiriki.hivyo wanafunzi wote wa kidato cha tano huchangia mahafali kwa kiwango kidogo ukilinganisha na kidato cha sita na pia atakapofika kidato cha sita atachangia mahafali kama muhusika mkuu.kwa muktadha huo,unapaswa kuchangia mahafali

Shule pia ina utaratibu wa mitihani ya kila mara kwa kidato cha tano na sita **(series exams)** ambayo wazazi huchangia ili angalau mtoto anapokuwa kidato cha tano apate mitihani kumi kwa kila somo. Mtihani hiyo ni tofauti na mitihani ya utaratibu wa kawaida ikiwemo **mid –term**, **TAHOSSA, terminal** n.k. lengo ni kumfanya mwanafunzi afanye mitihani mingi kwa kadri iwezekanavyo ili kuwa na maandalizi ya kutosha kwa mtihani wa Taifa kidato cha sita.

**4. SARE YA SHULE**

Suruali mbili rangi ya kaki za kuvaa darasani na suruali mbili rangi ya blue bahari (Light blue) za kuvaa baada ya masomo na kazi za nje, mshono marinda mawili mbele na chini turn up, uwe wa heshima isibane, iwe ndefu akivaa iguse viatu kifundo cha mguu.

a. Mashati meupe (**Tomato**) mawili (2) ya mikono mirefu ya kuvaa darasani.
b. Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (2).
c. Koti la suti la rangi ya kaki kwa ajili ya kuvaa darasani siku ya jumatatu na wakati wa baridi.
d. Aje na **Tai nyeusi** ndefu atakayo vaa wakati amevaa sare ya kaki
e. Viatu vyeusi vya kamba jozi mbili visiwe na urembo
f. **Truck Suit** ya rangi nyeusi kwa ajili ya michezo na kuvaa usiku wakati wa kujisomea (preparation).
g. Bukta moja ya bluu kwa ajili ya michezo
h. Nguo moja ya kulalia yoyote nyepesi (**Pajama)**

**5. MAHITAJI MENGINE**

a. Bunda (Ream) za karatasi mbili (2) kwa mwaka (**aina ya ream iwe Aone**).
b. Raba nyeupe za michezo jozi moja (1).
c. Shuka mbili (2) za rangi ya blue.
d. Godoro moja la ukubwa wa $2\ ^1/_2$ x 6
e. Mto na foronya.
f. Chandarua ya kuzuia mbu rangi nyeupe.
g. Sanduku la bati (Trunker).
h. Ndoo 2 (**ndoo 1 KUBWA** ya kuwekea maji ya kunywa na **ndoo 1 NDOGO** ya kuogea/kufulia)
i. **Vyombo vya kulia chakula (sahani ya bati yenye vyumba vyumba, kikombe na kijiko) na Tochi ya betri au taa ya Solar kwa tahadhari ya umeme ukikatika**.
j. Madaftari makubwa (counter book quire 3) sita (6) na faili ngumu kwa ajili ya **portfolio.**
k. Kitambulisho cha **bima ya afya au sh. 10,000/=** kwa ajili ya kuombewa bima ya afya.
l. Vifaa vya usafi: kwanja, sabuni ya maji (**TARMO 5ltr)**, panga na softbroom **(usilete fedha).**

**7. MENGINEYO**

a. Ni jukumu la mzazi/ mlezi kugharamia usafiri wa mwanafunzi kwenda na kurudi shuleni wakati wa likizo, pia awe na fedha za kujikimu awapo shuleni
b. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa shuleni.**

Nakutakia maandalizi mema, na karibu sana Kwala sekondari

HEADMASTER
KWALA SECONDARY SCHOOL
P.O. Box 05, MLANDIZI

**FERUZI S NANDALA**
**MKUU WA SHULE**

- **TSHIRT ANAZOTAKIWA KUWA NAZO NI;**
  a. Tshit ya blue maasai ya kuvaa shuleni siku ya Jumatano na Ijumaa

**Bluu Masai**



b. Tshirt ya kijivu ya kushindia

**Kijivu**



**NB: Mzazi/mlezi anapaswa kuzinunua T shirts zote 2 alafu nembo na maandishi vitafanyika shuleni**

Kiambatanisho A

**STUDENT'S MEDICAL EXANINATION FORM.**

**TO THE MEDICAL OFFICER IN CHARGE**

……………………………………………..

…………………………………………….

…………………………………………….

Please, examine the under named student and note any medical complications towards her joining this school.

Student's name …………………………………………………………………age …………… Class

1. Blood (any infection noted) ……………………………………………………………….
   Blood group…………
2. Stool …………………………………………………
3. Urine analysis………………………………………………………………………………...……
4. Eyes (any eye defect)…………………………………………………………..………
5. Ears (hearing strength)………………………………………………………..…………..………
6. Chest……………………………………………………………………………..………….
7. Abdomen……………………………………………………………………….………………
8. Hearing diseases ……………………………………………………………………………..…

Any chronic complaints which needs attention of the school authority

………………………………………………………………………………..…………………………

…………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………

**Name of the medical officer ………………………………………………………..**

**Designation ………………………………………………….….… Signature ……….…………………**

**Station ………………………………………………………..        Date ……………………………**

**Official stamp ………………………**

Kiambatanisho B

**(ANUANI YA MZAZI)**

………………………………………………………………

………………………………………………………………

………………………………………………………………

**YAH: <u>HATI YA KUKUBALI MASHARTI KUHUSU MWANAFUNZI</u> KUSOMA<u> SHULE YA SEKONDARI KWALA</u>**

Mimi ………………………………………………………………………..………… (Jina la Mzazi/ Mlezi wa mwanafunzi), Mzazi/ Mlezi wa ……………………………………...……………….(jina la mwanafunzi).

Aliyekuwa akisoma shule ya ……….……………………………………………. (taja jina la shule aliyosoma mwanafunzi) katika wilaya ya ……………………… Mkoa wa ………………………

Ninakubali mwanafunzi asome shule ya sekondari

Kwala iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha na nitazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule kama atakavyo elekezwa na walimu na kwamba:-

1. Mwanafunzi atahudhuria masomo kama kawaida na kufanya shughuli nyingine zote za shule akikaa shuleni/ nyumbani kwa kipindi chote cha miaka miwili cha kidato cha tano hadi cha sita,

2. Kwa muda wote huo wa miaka miwili sitamsumbua Mkuu wa shule, Afisa Elimu Sekondari Wilaya na Mkoa kuomba uhamisho.

………………………………  ……………………….

**SAHIHI YA MZAZI**  **TAREHE**

Kiambatanisho C

**FOMU YA KIAPO CHA MWANAFUNZI CHA KUTOSHIRIKI MIGOMO, FUJO PAMOJA NA MAKOSA YA JINAI.**

Mimi…………………………………………………….……………………………………...….……
Nimekubali nafasi niliyopewa katika shule ya sekondari Kwala ninaahidi kuwa mtiifu na kufuata kikamilifu **SHERIA, KANUNI** na **TARATIBU** halali zilizopo. Pia ninaahidi kufanya bidii na kushirikiana na uongozi was hule na wanafunzi wenzangu katika kuendeleza taaluma na shughuli nyingine nitakazo pangiwa. Naahidi kutoshiriki katika migomo, fujo pamoja na makosa ya jinai.

**JINA LA MWANAFUNZI** **SAHIHI**

…………………………………………… …………………………

Tarehe: ……………………………………..……..………..

**Kiambatanisho D**

**FOMU YA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI**

1. Jina kamili la mwanafunzi………… ……………………………..

Dini ……………………………………………….

2. Tarehe ya kuzaliwa…………..…………….Mahali alipozaliwa ……...……………
3. Jina la Baba ………….…………………………………Hai/amefariki
4. Jina la Mama ……………………………….Hai/amefariki
   (a) Je unaishi na wazazi wako? Ndiyo/Hapana
   (b) Kama hapana. Je unaishi na nani? Jina

   ………………………………………………………………….…………………

   Uhusiano ……………….…………………..
5. Kidato unacho kuja kuingia hapa shuleni ……………………………………..……
6. Michezo/ngoma unazopendelea hapa shuleni ………………………………………
7. Je umewahi kuwa kiongozi/Kiranja? Ndiyo/Hapana. Kama jibu ni ndiyo eleza ulikuwa kiongozi/Kiranja wanini? ………………………………………………………………
8. Taja mambo mengine unayopendelea kufanya nje ya masomo.……………………………………..

   ……………………………………………………………………………………………………

9. **ORODHESHA MAJINA YA NDUGU WA KARIBU (WA KIKE/KIUME)**

| NA. | JINA LA NDUGU | UHUSIANO | KAZI YAKE | NA. YA SIMU |
|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | |
| 2. | | | | |
| 3. | | | | |
| 4. | | | | |
| 5. | | | | |

**Nathibitisha kwamba taarifa nilizotoa hapo juu ni sahihi.**

Sahihi ya Mwanafunzi_________________________ Tarehe:____________

**Kiambatanisho E**

**SHERIA ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa sharia Na 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayo tolewa na wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi wa uendeshaji Elimu.

Unatakiwa kuzingatia sheria, taratibu, na kanuni za shule kama ifuatavyo;

a) Heshima kwa walimu, viongozi,wazazi,wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Kuwa na mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje, kulingana na ratiba ya shule ikiwa ni pamoja na maandalio ya jioni (preparation).
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazo pewa
d) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapokuwa shuleni au safarini.
e) Kutunza mali ya umma
f) Kumwabudu Mungu kwa utaratibu wa vipindi vya dini vilivyopangwa na shule
g) Ni muhimu na wajibu wa kila mwanafunzi kutii kengele ya shule.
h) Ni marufuku kwenda kwenye nyumba za walimu bila kibali maalumu na kuonekana nje ya mipaka ya shule.
i) Ni marufuku kwa wanafunzi kuonekana kwenye nyumba za kulala wageni/gesti
j) Ni marufuku kwa mwanafunzi kutumia vipodozi vya aina yeyote na pafyumu.
k) Ni marufuku kwa mwanafunzi kuonekana ndani au maeneo ya mabweni ya jinsia tofauti
l) Ni marufuku kwa mwanafunzi kushiriki/kushawishi Vitendo vyovyote vya mgomo au aina yeyote vya kutowesha Amani shuleni.
m) Ni marufuku kwa mvulana na msichana kukutana wakati wa usiku isipokuwa ikilazimu Mkuu wa shule atatoa kibali.

**MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE/KUSIMAMISHWA MASOMO.**

i. Wizi
ii. Uasherati na ushoga
iii. Ubakaji
iv. Ulevi
v. Kupigana na kupiga
vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
vii. Kudharau bendera yaTaifa
viii. Kuoa /kuolewa
ix. Kutoa mimba
x. Kuwa na simu ya mkononi
xi. Kukataa adhabu kwa makusudi
xii. Kugoma, kuchochea, kuongoza na kushiriki kuvuruga Amani na usalama was hule au watu.

**Kiambatanisho F**

# VITABU

## 1. ENGLISH

1. **ANIMAL FARM BY GEORGE ORWELL(2024)**
2. **CHASING THE LEOPARD FINDING THE LION BY JULIE WAKEMAN(2024)**
3. **THE OPPORTUNIST ELITE BY NYAMBARI NYANGWINE (2023)**
4. **THE HORIZON UNVEILED BY FELLOWES MWAISELA (2011)**
5. **THE GOVERNMENT INSPECTOR BY NIKOLAI GOGOL (2024)**
6. **AN ENEMY OF THE PEOPLE BY HENRICK IBSEN (2024)**
7. **A TASTE OF HEAVEN BY FAROUK TOPAN (2023)**
8. **SUMMONS POEMS FROM AFRICA BY RICHARD S MABALA(2023)**
9. **POETS OF AFRICA LAMENT OF THE SILENT BY JARED ANGIRA (2024)**

2. **KISWAHILI**

1. **DUNIA UWANJA WA FUJO BY EUPHRASE KEZILAHABI (2023)**
2. **UA LA FARAJA BY W.E MKUFYA (2007)**
3. **MIRATHI YA HATARI BY C.G MUNG'ONG'O (2023)**
4. **WASIFU WA SITI BINT SAAD BY SHABAAN ROBERT (2023)**
5. **MUKWAVA WA UHEHE BY M.M. MULOKOZI (2023)**
6. **SHUJAA MIRAMBO BY EMANUEL MBOGO (2023)**
7. **USALITI MJINI BY FRANCIS IMBUGA (2024)**
8. **FUMBO LINALOELEA BY NYAMBARI NYANGWINE (2023)**
9. **MALENGA WA ZIWA KUU BY WALLAH BIN WALLAH (2024)**
10. **ANDAMO MSAFIRI SAFARINI BY MOHAMED GHASAN (2024)**
11. **WOSIA WA BABA BY AHMED M AMANZY (2024)**

**3 HISTORY**

1. **HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS, NEW SYLLABUS FORM FIVE.TIE 2024**
2. **HISTORY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS, NEW SYLLABUS FORM SIX TIE 2O25**